

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBAHA



Kumb.Na: KDC/L.40/21/112

01/06/2023.

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha imepokea kibali cha ajira mpya kwa mwaka wa fedha 2022/2023 chenye Kumb. Na. FA.170/375/01”B”/138 cha tarehe 08 Mei, 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora.

Kupitia kibali hicho, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Kibaha anapenda kuwatangazia wananchi wote kuomba nafasi hizo kama zilivyoorodheshwa hapa chini.

1. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II. *NAFASI TATU. (03)*

A. SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na Elimu ya kidato cha Nne (Form IV) au Kidato cha Sita (Form VI) aliyehitimu mafunzo ya Stashahada/Diploma (NTA Level 6) katika fani ya Masijala katika vyuo vinavyotambulika na Serikali.

B. KAZI NA MAJUKUMU YA MTUNZA KUMBUKUMBU DARAJA LA II

- Kuorodhesha barua zinazolingia masijala kwenye Regista (Incoming Correspondence Register)
- Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya Taasisi (Outgoing Correspondence Register)
- Kusambaza Majalada kwa Watendaji (Action Officers)
- Kupokea Majalada yanayorudi Masijala kutoka kwa Watendaji
- Kutafuta kumbukumbu/Nyaraka au majalada yanayohitajika na Watendaji.
- Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada (Racks/Filing Cabinets) au mahali pengine yanapohifadhiwa.
- Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani na nje ya Taasisi (File tracking)

Mshahara: Ngazi ya mishahara ya Serikali ya **TGS C** kwa mwezi.

C. MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI:


- Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi 45.
- Awe raia wa Tanzania.
- Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya kidato cha IV au VI, cheti cha kuzaliwa na picha moja ya rangi za hivi karibuni katika barua ya maombi, pamoja na nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA)
- Aambatanishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba za simu zilizosajiliwa kwa majina yake kamili, ikiwa ni pamoja na wadhamini wawili na anuani zao kamili.
- Aambatanishe picha mbili “Passport size” za hivi karibuni na kuandika majina yake.
- Uwasilishwaji wa tarifa na sifa za kugushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria

- Waombaji wenye vyeti vya ngazi ya NTA Level 5 (Technician Certificate) maombi hayo hayatafanyiwa kazi. Cheti kinachopokelewa na kufanyiwa kazi ni NTA Level 6 (Diploma Certificate)
- Watakaofaulu kuitwa kwenye usaili, majina yao yatawekwa kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya Kibaha yaani: www.kibahadc.go.tz na Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira yaani: www.ajira.go.tz
- Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 14 Juni 2023 saa 9:30 Alasiri

Tangazo hili linapatikana pia katika Tovuti ya Halmashauri, yaani www.kibahadc.go.tz na Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira yaan: www.ajira.go.tz

Maombi yote yatumwe kwa Anuani ifuatayo:

Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya
S.L.P 30153
KIBAHA.



Emmanuel Mkwe
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KIBAHA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
KIBAHA